


JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI
WAKALA WA VYUO VYA MAFUNZO YA MIFUGO



MINYOO YA KUKU

Kimetayarishwa na:

Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA)
Kampasi ya Morogoro
S.L.P. 603,
MOROGORO – TANZANIA
E-mail: litamorocamp@gmail.com

UTANGULIZI

Minyoo ya kuku ni hatari kwani huleta hasara kubwa kwa mfugaji wa kuku wa nyama na mayai. Minyoo husababisha vifo vingi kwa kuku na hivyo kumkosesha kipato na mtaji mfugaji. Hata hivyo; licha ya madhara lukuki, ni wakulima wachache mno huchukua hatua mahusisi za kulikabili na kuthibiti tatizo hili.

AINA ZA MINYOO YA KUKU

- MINYOO MVIRINGO
- MINYOO BAPA

MINYOO MVIRINGO

- *Ascaridia galli*
 - -Ni mkubwa kuliko minyoo mviringo yote ya kuku.
 - -Hupatikana katika utumbo
 - mwembamba wa kuku
 - -Ipo aina dume ya minyoo yenye urefu
 - yapata sm 3 hadi sm 8 na minyoo ya
 - kike yenye urefu wa sm 6 hadi sm 12.
- *Heterakis gallinae*
 - -Hupatikana katika utumbo mpana.
 - -Minyoo dume ina urefu wa mm 4 hadi
 - mm 13 na ya kike ina urefu wa mm 8
 - hadi mm15.
- *Syngamus trachea*
 - Hupatikana kwenye koo
 - Minyoo jike ina urefu wa mm 25 hadi
 - mm 40. Minyoo dume huwa na urefu
 - mm 2 hadi mm 6.
- *Oxyspirura mansoni*
 - Hupatikana kwenye macho (conjunctival
 - sac)
 - Minyoo jike ina urefu wa mm 12 hadi
 - mm 19.
- *Gongylonema ingluvicola*
 - Hupatikana katika umio au gole la
 - ndege.
 - Minyoo jike ina urefu ya pata mm 32
 - hadi mm 55.
- *Cheilospirura hamulosa*

- Hupatikana kwenye firigisi.

Minyoo jike ina urefu wa mm 16 hadi mm 25.

- *Tetrameres americana*
 - Hupatikana karibu na firigisi
 - Minyoo jike huwa na urefu wa mm
 - 3.5
 - hadi 4.5
- *Dyspharynx nasuta*.
 - Hii pia hupatikana kwenye firigisi,
 - minyoo hii hukua na kufikia mm 10
 - kwa ile ya kike.

TEGU WA KUKU

- Minyoo hii hupatikana kwenye utumbo mwembamba.
- Huathiri kuku na jamii ya ndege.
- Kuku hupata aina hii ya minyoo kwa kula wadudu wabebao mayai au viini vya minyoo. Mfano minyoo ardhi (earthworms), konokono, inzi n.k.
- Ina umbo bapa.

➤ *Raillietina tetragona*

- Urefu hadi sm 25
- Wanapatikana kwenye utumbo
- mwembamba

➤ *Raillietina echinobothridia*

- Urefu hadi sm 25
- Mahali, utumbo mwembamba.

➤ *Raillietina cesticillus*

- Urefu hadi sm 13
- Mahali utumbo mwembamba

➤ *Davainea proglottina*.

- Urefu hadi mm 3
- Mahali, utumbo mwembamba

➤ *Amoebotaemia sphenoides*

- Urefu hadi mm 4
- Mahali, utumbo mwembamba

➤ *Choanotaenia infundibulum*

- Urefu hadi cm 30

1. UENEZWAJI WA MINYOO

- Kupitia chakula
- Kupitia ngozi

- Vilevile kuku kupata minyoo kwa kula wadu wabebao mayai au viini vya minyoo kama v Inzi, konokono n.k.

2. DALILI ZA MINYOO

- Kuku hukosa hamu ya kula
- Ukondefu
- Kushuka chini kwa utagaji wa mayai
- Kuku hunyongea
- Baadhi ya minyoo hukaba koo na kumfany kuku ashindwe kupumua
- Baadhi ya minyoo huleta muasho kweny macho.
- Minyoo pia huzuia mpito wa chakula na hivy kuleta njaa kwa kuku.
- Minyoo ikizidi huua kuku
- Kuku pia huweza kupatwa na maambukizo y magonjwa nyemelezi hasa pale minyoo inapotoboa utumbo na kusababisha vidonda: Bakteria huweza kushambulia sehemu hizi.
- Upungufu wa damu.

3. TIBA

- Minyoo mikubwa mviringo hutibiwa kwa daw aina ya
Piperazine – kwenye chakula au maji y kunywa
Treamisole – kwenye chakula au maji
- Minyoo ya kuku (syngamus strachea) hutibiwa kwa dawa aina ya:
 1. Thiabendazole
 2. Tetramisole
- Minyoo Bapa (Tegu wa kuku) hutibiwa na dawa zilizwayo Di-N-butyl tin dilaurate hi huchanganywa kwenye chakula.
- Minyoo macho (Oxyspirura mansoni) huondolewa kutoka kwenye konjakitiva ya macho kwa kutumia vifaa maalum kama vile kibanio (forceps)

**JINSI YA KUZUIA MAAMBUKIZI YA MIINYOC
KWA KUKU**

- Minyoo huweza kuepukwa kwa kuacha mfumo huria wa ufugaji wa kuku. Hivyo basi fuga kuku wako kwa kutumia mfumo wa ndani (Intensive system)
- Usafi (Hygiene), mrundikano wa kinyesi cha kuku na uwepo wa miozo ya vyakula huvutia inzi na hivyo inzi kuacha mayai na viini vya minyoo. Hivyo epuka uchafu kwenye banda la kufugia kuku wako.
- Zuia kuku wako wasile wadudu wabebao viini vya mayai ya minyoo. Zoezi laweze kuwa gumu, hata hivyo kuna dawa zinazwa kwenye maduka ya mifugo ambazo zinaua viini vya minyoo vilivyo ardhini
- Kwa ushauri zaidi onana na wataalam wa mifugo. HAKIKA watakushauri aina ya dawa na jinsi ya kuitumia.